

*Utenzi ufuatalo uliandikwa na Alhaji Sheikh Yusuf Kalala wakati wa Masiba wa Marehemu Dr. Rugatiri Mekacha ambaye alimkuwa Mwana-Tanzanet Mashuhuri na siku zote alikuwa mstari wa mbele katika matumizi sahihi ya klugha ya kiswahili. Dr. Mekacha alikuwa pia mjumbe wa kamati ya Tunu ya Kandoro ambayo inadhaminiwa na Tanzanet kwa ajili ya kuhamasisha uandishi na utunzi unaochochea fikra.*

### **Tumepigwa na Butwaa-Dr. Mekacha**

1. Casmir tumepokea,  
Habari ulotuletea,  
Rugatiri katupotea,  
Mara tuliposikia,  
Hudhuni imetuingia,  
Tumepigwa na butwaa.
2. Ugonjwa tuliusikia,  
Nguvu hazikutuishia,  
Dua tulimuombea,  
Afya njema kumtakia,  
Lakini hakuondokea,  
Tumepigwa na butwaa.
3. Mekacha katutangulia,  
Sote tulikoelekea,  
Majonzi katuachia,  
Sote tumejiinamia,  
Hatuna la kujiambia,  
Tumepigwa na butwaa.
4. Wengine hatukumjua,  
Sura yake kujionea,  
Lakini tulimkaribia,  
Kalamu tulipoitumia,  
Hatuna la kumfanyia,  
Tumepigwa na butwaa.
5. Ukumbini alipotokezea  
Sote tulifurahia,  
Umahiri alopangilia,  
Hekima zake murua,  
Hakuna wa kuelezea,  
Tumepigwa na butwaa.
6. Lugha alokitumia,  
Mno alijulia,  
Kiswahili asilia,  
Na Kiingerza pia,  
Hatuna wa kumfananishia,  
Tumepigwa na butwaa.
7. Pengo alotuachia  
Si rahisi kujazia,  
Chini tumejikalia,  
Vigumu kujiinua  
Hatuna la kufikiria,  
Tumepigwa na butwaa.
8. uzidi kumuombea,  
Huko alikoendea,  
Mola kumpokea,  
Pema kumwekea,  
Hatuna la kuzidishia,  
Tumepigwa na butwaa.
9. Na yake familia,  
Pole twawapelekea,  
Waweze kuvumilia,  
Msiba ulowafikia,  
Hatuna la kuwapozea,  
Tumepigwa na butwaa.

*Yusuf M. Kalala,  
Washington D.C.  
30<sup>th</sup> September 2001*